

**AE.464/687/01/69**

**16 April, 2024**

Ndugu wadau,

**KUH: RASIMU ZA VIWANGO KWA AJILI YA MAONI KWA UMMA**

Tafadhali husika na mada iliopo hapo juu.

Taasisi ya Viwango Zanzibar imeandaa rasimu **mbili (2)** za viwango kupitia Kamati ya kitaalamu ya ZBS ya **Huduma za Utalii**, hivyo, Taasisi inasambaza rasimu za viwango hivyo kwa ajili ya kupata maoni kwa wadau kabla ya kupitishwa na Bodi ya wakurugenzi ya ZBS na baadae kutangazwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda katika Gazeti la Serikali.

Viwango hivyo ni: -


- PCD 572: 2024 Tour operators - Code of practice
- PCD 574: 2024 Adventure tourism — Tour leader —Personal competency

Kulingana na taratibu za kuandaa Viwango, rasimu za viwango baada ya kuandaliwa na kamati za kitaalamu husambazwa kwa wadau kwa ajili ya kukusanya maoni na mapendekezo. Hivyo, tunakuomba upitie rasimu za viwango vilivyoambatanishwa na kutuma maoni yako ya kiufundi. Maoni ambayo yana marekebisho ya kimaandishi inapaswa kuonyesha mabadala wake/mapendekezo kwa kila kifungu husika. Ikiwa utaona rasimu hizo zinafaa na hakuna maoni yoyote, tafadhali tuarifu ipasavyo.

Maoni lazima yajazwe katika **fomu** iliyo ambatanishwa na kuwasilishwa moja kwa moja katika afisi ya ZBS au kwa barua pepe [maoni@zbs.go.tz](mailto:maoni@zbs.go.tz).

Tutashukuru kupokea maoni yako mapema, mwisho wa kupokea maoni ni tarehe **16 June, 2024**.

Asante.



**(Yussuph Majid Nassor)**  
**MKURUGENZI MKUU**  
**TAASISI YA VIWANGO**  
**ZANZIBAR**



**Mawasiliano yote yafanywe kwa Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Viwango Zanzibar**  
**Barua pepe: info@zbs.go.tz Simu: +255 24 2232225**

Zanzibar Bureau of Standards



[www.zbs.go.tz](http://www.zbs.go.tz)



[info@zbs.go.tz](mailto:info@zbs.go.tz)